NSSF EMPLOYEES CO OPERATIVE SAVINGS AND CREDIT SOCIETY LTD
MWALIMU NYERERE PENSION TOWER GHOROFA YA SITA
HATI NA. 2056: SLP 19910, EMAIL: saccosnssf@gmail.com
DAR ES SALAAM

TAARIFA YA UTENDAJI KWA MKUTANO MKUU WA HAMSINI NA MOJA TAREHE 09 DISEMBA, 2022 – KATIKA UKUMBI WA MAFAO HOUSE NSSF ILALA – DAR ES SALAAM

1.0 UTANGULIZI

1.1 Ndugu Mrajis msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Dar es Salaam,
Ndugu Maafisa Ushirika kutoka ofisi za Ushirika Halmashauri ya jiji la Ilala,
Ndugu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Hifadhi ya Jamii. (NSSF)
Ndugu mwakilishi kutoka SCCULT,
Ndugu Wageni waalikwa kutoka taasisi mbalimbali.
Ndugu Wawakilishi kutoka mikoa mbalimbali,
Habari zenu na karibuni sana katika mkutano wetu wa leo.

1.2 Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii Kwa niaba ya Bodi ya NSSF EMPLOYEES SACCOS kuwakaribisha wageni wetu na kuwashukuru kwa kukubali kuacha majukumu yenu mengine na kuja kujumuika nasi leo. Tunashukuru sana kwa heshima mliyotupa, tunasema asanteni sana na karibuni mshirikiane nasi katika mkutano huu wa hamsini (51) wa NSSF EMPLOYEES SACCOS.

1.3 Ni faraja kubwa kwetu kukutana pamoja tena leo hii. Hakika ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake zilizotuwezesha kukutana hapa leo tukiwa wazima na afya njema.

1.4 Kwa masikitiko makubwa napenda kuchukua nafasi hii kuwakumbuka wanachama wenzetu wawili [2] ambao wamepoteza maisha katika kipindi cha mwaka 2022 kama inavyo onyesha katika jedwali hapa chini.

WANACHAMA WALIOFARIKI JANUARI – SEPTEMBA 2022			
S/No.	**JINA**	**NAMBA YA UANACHAMA**	**MKOA/OFISI**
1	GABRIEL CEASER	1940	MBEYA
2	ASANTINA YOLA		DSM

Naomba tusimame Kwa dakika moja kuwakumbuka wenzetu waliotangulia mbele za haki "*EWE MWENYEZI MUNGU TUNAKUOMBA UWAREHEMU NA UWAPOKEE NA KUZIWEKA ROHO ZA MAREHEMU HAWA MAHALI PEMA PEPONI – AMEEN".*

2.0 TAARIFA YA UTENDAJI KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI SEPTEMBA 2022

2.1 Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu, napenda kueleza kuwa taarifa hii inaelezea utendaji wa shughuli za Ushirika katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka 2022 yaani kutoka Januari – Septemba, 2022

2.2 Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu, napenda kuwaeleza wanaushirika wenzangu kwamba katika kipindi cha mwaka 2022 kulikuwa na mafanikio na changamoto kama taarifa hii itakavyoeleza.

3.0 Taarifa za Wanachama

3.1 Idadi ya wanachama

Ndugu Wajumbewa Mkutano Mkuu**,** mpaka kufikia Septemba 2022 jumla ya wanachama hai tuliokuwa nao ni ni 300 ikilinganishwa na wanachama 264 waliokuwapo katika kipindi kilichoishia Disemba 2021.

Kama takwimu zinavyoonyesha, idadi ya wanachama waliongezeka ni 47. Bodi inatoa rai kwa wajumbe kila mmoja kwa nafasi yake afanye juhudi za makusudi kushawishi na kuelimisha wafanyakazi ambao bado hawajajiunga na Ushirikana wale waliojitoa kurudisha tena uanachama wao. Vile vile Bodi inashauri pia kushawishi wanachama waliopo katika harakati za kutojitoa katika Ushirika wetu kwani yajayo yanafurahisha.

3.2 Wanachama Wapya

Katika kipindi cha Januari – Septemba, 2022 jumla ya wanachama [39] wamejiunga na Ushirika wetu na wengine [08] kuamua kuhuisha uanachama wao baada ya kupata elimu juu ya faida za kujiendeleza na uanachama wao, ukilinganisha na wanachama kumi na saba[17], waliojiunga na ishirini na tatu(23) waliohuisha uwanachama wao katika mwaka 2021. {***Kiambatisho Na 1}***.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha wanaushirika wapya ambao wameona umuhimu na kuchukua uamuzi huu wenye busara wa kujiunga na Ushirika wetu.

3.3 Wanachama Waliojitoa

Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2022 jumla ya wanachama [09] walijitoa katika Ushirika kwa sababu mbalimbali, ukilinganisha na wanachama kumi na nane [18] waliojitoa katika Ushirika kwa mwaka 2021. **[Kiambatisho 2]**

3.4 Malipo ya waliojitoa uanachama kuanzia Januari – Septemba 2022

Kipindi cha Januari mpaka Septemba 2022 jumla ya wanachama 71 walilipwa stahiki zao za kujitoa zenye thamani ya Tshs 123,196,315.85 ukilinganisha wanachama 81waliolipwa jumla ya Tshs 123,747,231.37 katika kipindi cha Januari mpaka Disemba 2021.

Kwa ujumla malipo kwa waliojitoa toka mwaka 2016 mpaka Oktoba 2022 ni shilingi 1,638,644,997.99.

Bado kuna wanachama wanaofikia 149 ambao hawajalipwa stahiki zao ambazo zinafikia kiasi cha Shilingi 447,274,486.03

Kuchelewa kuwalipa wanachama waliojitoa inasababishwa na kujitoa kwa wanachama kwa wingi kwa mara moja hivyo kufanya Ushirika ushindwe kuwalipa wote kwa mara moja na wakati huo huo kuendelea kutoa mikopo kwa wanachama wake ambao ndio jukumu lake la msingi.

3.5 **Akiba za Wanachama**

Ndugu wajumbe wa Mkutano Mkuu, mpaka kufikia Septemba 30, 2022 Akiba za wanachama zimefikia Tshs 2,511,004,463.49, ikiwa ni ongezeko la Tshs 169,363,512.96 ukilinganisha na Akiba za Tshs 2,341,640,950.53 za mwaka 2021.

3.6 **Hisa za Wanachama**

Ndugu wajumbe, mpaka kufikia Septemba 30, 2022 Hisa za wanachama zimefikia Tshs 347,075,068.27ukilinganisha na Hisa za Tshs. 344,973,468.27 zilizokuwepo Desemba 2021. Hili ni ongezeko ya Tshs 2,101,600.00 Hali hii ya kuongezeka kwa fedha za Hisa imechangiwa na kujiunga kwa wanachama.

4.0 Taarifa ya Mikopo

4.1 **Utoaji wa Mikopo**

Ndugu wajumbe wa Mkutano Mkuu, jumla ya mikopo 250 yenye thamani ya Tshs 650,329,750.00 ilitolewa katika kipindi cha Januari – Septemba 2022 ukilinganisha na mikopo 156 yenye thamani ya Tshs 470,869,637.35 iliyotolewa mwaka 2021.

Ndugu wajumbe mtabaini kuwa pamoja na wanachama kujitoa kwa idadi kubwa bado Ushirika wetu umeendelea kutoa mikopo kwa kiasi kikubwa kama ifuatavyo:-.

i) **Mikopo ya maendeleo**

Katika kipindi cha Januari – Septemba 2022 mikopo ya maendeleo ilikuwa 83 yenye thamani ya Tshs 423,499,750.00 ukilinganisha na mikopo ya maendeleo 74 yenye thamani ya Tshs 289,446,637.65iliyotolewa katika kipindi cha mwaka 2021.

ii) **Mikopo ya dharura**

kwa kipindi cha Januari – Septemba 2022 mikopo ya dharura ilikuwa 66 yenye thamani ya Tshs 108,440,000.00 ukilinganisha na mikopo 82 yenye thamani ya Tshs 181,423,000.00 iliyotolewa mwaka 2021

iii) Mikopo ya chap chap

Kwa kipindi cha januari – Septemba 2022 mikopo ya chap chap ilikuwa 57 yenye thaman ya Tshs 27,040,000.00

iv) Mikopo ya elimu

Kwa kipindi cha januari – septemba 2022 mikopo ya elimu ilikuwa 26 yenye thamani ya tshs 43,400,000.00

v) Mikopo ya CFF

Kwa kipindi cha januari – septemba 2022 mikopo ya cff ilikuwa 9 yenye thamani ya Tshs 45,000,000.00

vi) Mikopo ya sikukuu

Kwa kipindi cha januari – September 2022 mikopo ya sikukuu ilikuwa 5 yenye thamani ya Tshs 1,300,000.00

vii) Mikopo ya mazishi

Kwa kipindi cha januari – septemba 2022 mikopo ya mazishi ilikuwa 2 yenye thamani ya Tshs 1,000,000.00

viii) Mikopo ya bima

Kwa kipindi cha januari – septemba 2022 mikopo ya bima ulikuwa 1 wenye thamani ya Tshs 450,000.00

ix) Mikopo ya weekendi

Kwa kipindi cha januari – septemba 2022 mikopo ya weekend ulikuwa 1 wenye thamani ya Tshs 200,000.00 {**kiambatisho 3**} vinaonyesha idadi na kiwango cha mikopo kwa kila mwezi

4.2 **Marejesho ya mikopo**

Katika kipindi cha Januari – Septemba, 2022 marejesho ya mikopo yalikuwa jumla ya Tshs 456,328,048.04 ukilinganisha na Tshs 405,147,451.53 zilizorejeshwa mwaka 2021. ***Kiambatisho [4]*** kinaonyesha kwa mwezi na kiasi kilichorejeshwa kupitia makato ya mishahara na malipo kupitia Benki***.***

5.0 Taarifa ya Hesabu za mwaka 2021

Ndugu wajumbe, Ukaguzi wa Hesabu za Mwaka 2021 uliofanywa na COASCO umekamilika hivyo hesabu hizo zitawasilishwa kwenu na wakaguzi kutoka COASCO na kujadiliwa katika mkutano huu.

6.0 Mtaji wa ushirika

Kwa miaka mingi chama chetu kimeKabiliwa na changamoto ya kutokuwa na mtaji unaoonekana (tangible share capital), Kwa kushirikiana na Benki ya Azania tumefanikiwa kuwa na mtaji unaoonekana ambao hadi sasa ni TZS 180,000,000.00 ambalo ni jambo la mafanikio kwetu.

7.0 Mikopo kutoka Taasisi za Fedha

7.1 Mkopo wa NSSF

Ushirika wetu ulikopa jumla ya Tshs 2,078,577,333.45 kutoka NSSF tangu mwaka 2004. Mpaka kufikia tarehe ya mkutano huu tumeweza kurejesha na tumebaki na deni la Tshs 246,953,833.00ukilinganisha na deni la Tshs 290,553,833.45lililokuwepo mwezi Disemba 2021

Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2022 tumeweza kurejesha jumla ya Tshs 36,600,000.00 ukilinganisha na Tshs 42,000,000.00 zilizorejeshwa mwaka 2021.

7.2 Mkopo wa SCULLT, ushirika wetu ulipata jumla ya Tshs 50,000,000.00 mnamo tarehe 09/03/2022 na kufanikiwa kurudisha jumla ya Tshs 24,377,718.34 Tumebaki na deni la Tshs 25,622,281.66

7.3 Mkopo wa benki ya AZANIA

Mwezi wa (4) tulifanikiwa kupata mkopo kutoka benki ya AZANIA kiasi cha Milioni mia tatu (TZS 300,000,000.00) riba ya asilimia kumi na mbili (12) kwa kipindi cha miaka mitatu na kupewa kwa awamu tatu, awamu ya kwanza tarehe 13 Aprili 2022 kiasi cha Shilingi Milioni mia hamsini (TZS 150,000,000.00) awamu ya pili tarehe 15/09/2022 Shilingi Milioni mia moja (TZS100,000,000.00) na awamu ya tatu (TZS50,000,000.00) ambazo tulichukua kidogo kidogo kila kwenye uhitaji

8.0 Madeni Sugu

Ndugu wajumbe wa Mkutano Mkuu, swala la madeni sugu bado linaendelea kutafutiwa ufumbuzi wakati bado bodi inaendelea kutafuta kampuni ya kukusanya madeni sugu baada ya kampuni ya awali iliyopewa kufanya kazi hiyo kutofanikiwa, bado marejesho ya madeni sugu haijawa ya kuridhisha kwani katika kipindi cha Januari – Oktoba 2022 tumefanikiwa kukusanya Tshs 3,120,000 tu kama ifuatavyo:-

NA.	PB NA.	JINA	KIASI(TSHS) KILICHOREJESHWA
1	371	MARY LUOGA	70,000.00
2	2536	RAMADHANI NJEMU	50,000.00
3	2238	SADI SHEMLIWA	1,000,000.00
4	1877	C. RWEYEMAMU	2,000,000.00
		JUMLA	**3,120,000.00**

Ndugu wajumbe madeni sugu hadi kufikia mwezi Septemba 2022 ni Tshs.62,099,065.68 ukilinganisha na kiasi cha Tshs 74,806,455.19 zilizokuwepo mwaka 2021. [***Kiambatisho 5].*** Sababu za kutofanikiwa katika zoezi la ukusanyaji wa madeni sugu ni pamoja na baadhi ya wadaiwa kutofahamika walipo na hata kwa wale wanaofahamika wakitafutwa kwa kupitia simu huishia kutoa ahadi ya kulipa ahadi ambazo hawazitekelezi.

Hivyo Bodi ya NSSF Employees SACCOS itaongeza juhudikatika mwaka wa fedha ujao kwazaidi kwa kutumia hatua za kisheria kuhakikisha cham kinakusanya madeni sugu kwa kutumia wakusanya kufuatilia madeni.

9.0 Mafanikio

9.1 Uwekezaji

Ndugu wajumbe wa Mkutano mkuu, katika kipindi cha Januari - Septemba 2022 chama kilifanikiwa kuwekeza katika benki ya Azania (FDR) hadi kufikia tarehe ya mkutano huu tumewekeza jumla ya TZS 180,000,000.00 (Milioni mia moja themani) mbali na uwekezaji huu pia chama kimewekeza kwenye hisa za Benki ya KCBL kiasi cha TZS. 2,000,000.00, SCULLT akiba kiasi cha TZS2,000,000.00, na hisa ya TZS. 200,000.00, na ELCT ND SACCOS akiba kiasi cha TZS.1,600,000.00 na hisa kiasi cha TZS.300,000.00 iliyopo mkoani Kilimanjaro

10.0 CHANGAMOTO

10.1 Mtaji mdogo

Kutokana na mtaji kuwa mdogo imepelekea chama kushindwa kukidhi mahitaji ya mikopo kwa wakati na utoaji wa mikopo mipya (ikiwemo bajaji na bodaboda), hivyo imechangia mapato kutoendana na matumizi.

10.2 Withdrawal

Ndugu wajumbe wa mkutano mkuu, bado kuna wimbi kubwa la wanachama wanaodai stahiki zao, hivyo kutokana na chama kutokuwa na mtaji wa kutosha imepelekea kupungua kwa kasi ya utoaji wa mikopo kwa wanachama hai ili kuwalipa wanaojitoa. Na pia bado kuna wanachama wanaotaka kujitoa.

10.3 Marejesho ya mkopo.

Ndugu wajumbe wa Mkutano Mkuu, kuna baadhi ya wanachama wamekuwa sio waaminifu hasa wanaolipia marejesho yao kwa fedha taslimu kwani wanashindwa kulipa marejesho yao kwa wakati, kwasababu

mbalimbali, kwa mfano: wanaweka standing order na tarehe inapofikia akaunti zao za benki zinakuwa hazina hela, wengine huahidi kuweka fedha taslimu kwenye akaunti ya chama lakini hawatimizi ahadi zao pia wengine wanaomba kufuta mikopo yao pindi watakapo pata mkopo kutoka kwa majiri. Na kupelekea chama kutofikia malengo yake.

10.4 **Upatikanaji wa taarifa za kibenki**

Kumekuwa na ucheleweshaji wa uwasilishwaji wa taarifa za kibenki kutoka kwa wanachama ambao leja zao zina miamala yenye utata, na baadhi yao ni viongozi ambao wako kwenye mkutano huu.

10.5 **Bodi Kushitakiwa na kutishiwa kushitakiwa Mahakamani**

Chama kimeshitakiwa Mahakamani na Wanachama wawili, ndugu Bertha Komba na Mohamed Mwalinde. Kesi ya ndugu Bertha komba tulishindwa na kuamriwa kumlipa ndani ya Miezi Mitatu. Pia ndugu Hussein Kaheka, James Msechu na Anold kileo walitishia kukipeleka Chama Mahakamani kwa Chama kushindwa kuwalipa kama walivyokuwa wameahidiwa.

11.0 UTATUZI WA CHANGAMOTO

11.1 Bodi inapendekeza wawakilishi kufanya juhudi ya kuongeza wanachama na ikiwezekana waajiriwa wote wa NSSF wajiunge na chama. Pia bodi iko katika mazungumzo na wadau mbalimbali na benki ya Azania imeonyesha nia ya kugharamia mikopo hiyo na mingineyo. Pia bodi ipo katika utafiti na mazungumzo na makampuni ya magari ya BEFOWARD na SBT.

11.2 Bodi inapendekeza kuwekeza nguvu katika utoaji wa elimu katika mikoa mbali mbali juu ya faida za chama ili kurudisha, kubakiza na kuongeza wanachama wapya ambao watasaidia kukuza chama. Hii itasaidia kuwalipa wale wanaodai stahiki zao.

11.3 Bodi inapendekeza kuwa marejesho yote yalipwe kwa wakati, pia marejesho ya mikopo mikubwa yote yapitie kwenye mishahara, na midogo chini ya TZS. 3,000,000.00 (milioni tatu) ilipwe kupitia fedha taslim.

11.4 Bodi inawaomba wanachama waliotakiwa kuwasilisha taarifa za kibenki waziwasilishe mapema ili kuweka kumbukumbu sahihi za mali(assets) za chama, kuweka kumbukumbu sahihi za taarifa za wanachama (hisa, akiba na mikopo), kutuwezesha kupata mapema fidia kutoka CRDB.

11.5 Katika kesi mbali mbali, Chama kimeweza kuingia makubaliano na ndugu Bertha komba (Settlement Agrement out of the Court) na ndugu Mwalinde kwa kuzitoa kesi nje ya mahakama na wanalipwa kidogokidogo. Pia Chama kimeweza kuzuia Kesi za ndugu Hussein Kaheka, James Msechu na Anold kileo kutokwenda Mahakamani na kuingia nao mikataba kwa ndugu Hussein Kaheka kulipwa kidogo kidogo, James Msechu, kupunguza Akiba na kuwa mwanachama na ndugu Kileo kuwa Mwanachama na kuchukua Mkopo.

12.0 MATARAJIO YA MWAKA 2023

12.1 Kushawishi wanachama wapya angalau mia tatu kujiunga na SACCOS yetu pia wanachama ambao walijitoa wahuishe uanachama wao ili kuongeza idadi ya wanachama itakayopelekea kuongezeka kwa mtaji wa chama na kutuwezesha kufikia ndoto zetu.

12.2 Kuhakikisha huduma ya mikopo inatolewa kwa wingi, kwa ubora na kwa wakati ili kuleta tija na ufanisi kwa wanachama na Ushirika kwa ujumla.

12.3 Kuendelea kutoa huduma kamili kupitia Tehama.

12.4 Kuendelea kukuza mtaji wa chama kwa kuhamasisha wanachama kuweka amana na hisa za hiari pia kwa kutumia mitaji isiyo na gharama na hata

yenye gharama nafuu. Pia endapo Chama kitapata pesa za kutosha kutoka CRDB, Bodi inaomba kibali, irushiwe kuendelea kutunza Mtaji Tete(Share Capital) katika mali halisi kwa njia ya Dhamana za Serikali za muda mrefu (Treasury Bonds), badala ya uwekezaji wa Muda maalumu (Fixed Deposit).

12.5 Bodi itajitahidi na kuhakikisha kuwa, inaongea na kuingia makubaliano na wanachama mbalimbali wenye madni yao mbalilmbali, ili kuzuia madai mbalimbali yasifike mahakamani.

13.0 SHUKRANI

Ndugu wajumbe, kwa niaba ya Bodi na kwa niaba yangu binafsi, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Bodi ya Wadhamini ya NSSF na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) pamoja na Menejimenti yote kwa ushirikiano tunaopata kutoka kwao.

14.0 HITIMISHO

Ndugu wajumbe kwa kumalizia, naomba tuwe wabunifu na washauri wazuri ili kuhakikisha Ushirika wetu unasonga mbele.

Hivyo naomba muipokee, muijadili na muitolee maelekezo taarifa hii.

Ahsanteni kwa kunisikiliza

Julius Ngonyani Shauritanga
MWENYEKITI WA BODI

09/12/2022